

Kujiandikisha

Karibu katika maktaba!

Tumefurahi sana kwa vile umetutembelea. Wakati maktaba imefunguliwa unaweza kutumia vitabu na vyombo vingine vyote viliyomo.

Katika maktaba yetu unaweza kuazima vitu vifuatavyo:

- Vitabu
- Majorida
- CD
- DVD

Kanuni za kuazima

Kwa kulipa karo ya mwaka ya 15 Euro unaweza kuazima vitabu na vyombo vingine. Watoto na vijana chini ya miaka 18 wanaruhusiwa kuazima vitabu bila malipo.

Ukitaka kuwekewa vitabu, lipa 1,50 Euro. Tutakujulisha punde tu kitabu hicho kimefika.

Kwa kujiandikisha unahitajika kuleta kitambulisho chako na pia kutupatia anwani yako unayotumia sasa.

Ikiwa watoto au vijana wanataka kujiandikisha, tunahitaji sahihi za wazazi au walinzi. Tafadhali tumia kwa uangalifu vitabu vyote unavyoazima. Ukipoteza au ukiharibu kitabu, utahitajika kulipa kingine kipyga.

Kurudisha vitabu

Unaweza kutumia vitabu ulivyoazima hadi tarehe ya kuvirudisha.

Rudisha vitabu na vitu vingine vyote ulivyoazima kwa wakati unaofaa, la sivo utapigwa faini.

Tunatumaini kuwa umeridhika na huduma zetu. Tutafurahi kama utawajulisha wengine kuhusu huduma hizi.

Idhini ya wazazi kwa watoto kutumia maktaba

Mtoto wako angependa kuazima vitabu kwa maktaba yetu. Tunahitaji idhini yako kama mzazi.

Mtoto wako aliye chini ya miaka 18 anaweza kutumia maktaba bila malipo. Mtoto wako akichelewa kurudisha vitabu alivyoazima atapigwa faini. Tafadhali hakikisha mtoto wako anatumia vitabu vya maktaba kwa uangalifu. Ukipoteza au akiharibu kitabu atahitajika kulipa kingine kipyga.

Tafadhali jaza kadi hii, weka sahihi yako na mpe mtoto wako airudishe kwa maktaba anapotutembelea tena.

Tungefurahi sana kama tungeweza kukukaribisha wewe pia katika maktaba yetu!